

ZAMA



ZETU

HOJA HUJIBIWA KWA HOJA...

NDANI

MAGUFULI KUTIKISA

Akizungumza na wafanyabiashara Magufuli atoa siku saba kwa waliokwepa kodi kujipeleka wenyewe vinginevyo sheria itawabana kokote waliko.

TAHARIRI: NI MAADUI?

Hatua mbalimbali zinazochukuliwa na Serikali ya Rais Magufuli linatufanya tuamini kuwa baadhi ya Watanzania siyo wenzetu!

OZ 2020: KUKATALIWA EL

Mtandao wa OZ ulishiriki kikamilivu kuwashawishi watu kumkataa Lowassa

KUFUMULIWA SERIKALI

Nyuma ya ucheleweshaji wa kutangazwa kwa Baraza la Mawaziri kuna makubwa zaidi. Kufumuliwa serikali nzima.

MIJADALA

Dhana ya "hapa kazi tu" inatekelezeka vipi katika nchi inayojaribu kujenga utawala wa sheria kama ya kwetu?

Disemba 4, 2015

Juzuu 2, Toleo la 2

MAGUFULI KUTIKISA TAIFA

• AWASHANGAA WATANZANIA • AWAPA CHANGAMOTO WAFANYABIASHARA

Rais wa Tanzania Bw. John Pombe Magufuli ameonesha mshangao wake wa jinsi gani taifa tajiri kama la kwetu limekuwa na umaskini wa kutisha. Rais Magufuli ameonesha mshangao wake huo katika mkutano wake na viongozi wa wafanyabiashara mbalimbali wa Tanzania ambao pia ulihudhuriwa na Makatibu Wakuu wa Wizara.

Rais Magufuli alitolea mfano wa jinsi gani taifa ambalo lina raslimali za kila namna kuwa taifa lisiloongoza katika sekta mbalimbali ambazo lina raslimali zake. Alishangaa iweke nchi kama India na Kenya ziweze kuongoza duniani kwa kuuza madini yaliyokatwa ya Tanzanite wakati madini hayo yanapatikana nchini.



Alishangaa pia kwa taifa ambalo linaweza kuwa na bidhaa nyingi zinazotokana na zao la ngozi inakuwaje hata viatu vya ngozi tunaagiza toka nje. Kwamba, hata maziwa ambayo yanapatikana kwa wingi nchini kuna maeneo kama Arusha ambapo maziwa hupelekwa Kenya

kwa ajili ya kuwekwa kwenye vikatoni mbalimbali na kusindikwa.

"Unajua wenzetu wanatucheka, wanatuona sisi tuna matatizo gani" alisema Rais Magufuli kwa mshangao. "Serikali tupo, sekta binafsi ipo, Tanzania business

TAHARIRI: HAWA WALIKUWA NI MAADUI WA TAIFA LETU

Tukisema walifanya Tanzania shamba la bibi tutakuwa tumewapa heshima kidogo. Kwenye shamba la bibi mtu anaweza hata kuogopa kidogo; well cha 'bibi' ni chetu pia. Shamba la bibi utalima, utapanda na kupalilia, na hata ukila zaidi hutakula kama una ugomvi na nyanya'ako.

Hawa waligeuza Tanzania siyo shamba la bibi; labda tuseme waligeuza shamba la jirani. Lakini hata jirani kama ni mzuri na mnaishi vizuri

huwezi kuharibu shamba lake na kula hadi mbegu. Jirani ambaye mnaliandiana nyumba na mnasaidiana huwezi kumharibia shamba lake hivyo. Hawakulifanya kuwa ni shamba la bibi wala la jirani.

Waligeuza Tanzania kama shamba la adui; adui ambaye hawakuweza kumvumilia; adui ambaye walimchukulia. Mtu ambaye hakustahili hata chembe ya mapenzi yao kwake. Wakati wengine tunapoimba

"Tanzania Tanzania nakupenda kwa moyo wote" wao wanaimba mioyoni "Tanzania nakuchukia". Hawatasema hivyo wazi lakini vitendo vyao vinathibitisha. Mtu mwenye mapenzi hata ya mbali kwa nchi yake hawezi kufanya ambayo hawa wamefanya.

Tanzania ni shamba letu, ni shamba la familia yetu, ni shamba la Watanzania wote na wote ni wote! Ni shamba la vizazi vya sasa na ni

MAGUFULI KUTIKISA TAIFA

council ipo, mawaziri wapo, makatibu wakuu wapo, Rais mimi nipo" alisema Rais akionesha kuwa hakuna sababu ya taifa letu kuwa katika hali yake ilivyo sasa hasa kama kila mtu atati-miza wajibu wake kwa uzalendo.

Rais alishangazwa kuona pia tangu bajeti ilipopitishwa miezi karibu sita nyuma hakuna hela yoyote ya maendeleo ambayo ilishapelekwa kwenye maendeleo. "Tangu bajeti kupitishwa mwaka huu 2015/2016 – hatajatolewa fedha yoyote kwa ajili ya mipango ya maendeleo; hata senti tano" alisema Rais Magufuli. Kwamba fedha kidogo iliyotolewa kwenda kwenye maendeleo imetolewa mwezi huu – yeye akiwa tayari Rais; yaani kwa karibu miezi sita fedha ambayo imekuwa ikitolewa ni kwa ajili ya kushughulikia bajeti ya mambo ya kawaida siyo ya mipango ya maendeleo. Alisema kuwa kwa mwezi huu wametoa karibu shilingi bilioni 120 hivi kwa ajili ya miradi mbalimbali ya maendeleo. Kwa maneno mengine, kwa karibu miezi sita hakukuwa na miradi ya maendeleo ambayo ilikuwa inalipiwa na fedha za bajeti.

Akizungumzia juu ya hatua mbalimbali ambazo serikali yake imechukua hadi hivi sasa, Rais Magufuli amesema kuwa hawafanyi hivyo kwa ajili ya jeuri bali ni kwa ajili ya nia nzuri ya kuhakikisha kuwa Watanzania – hasa wa kipato cha chini – waweze kupata kile wanachokihitaji. Aliahidi kutoa ushirikiano wake wote kwa wafanyabiashara wa Tanzania.

Rais Magufuli amewaambia wafanyabiashara hao kuwa hawam dai kitu chochote na kuwa hakuna anayeweza kusema kuwa alimchangia Magufuli ili aiingie Ikulu. "Nilijiepusha sana na fedha yoyote kutoka na mchango wa mfanyabiashara yeyote" alisema Magufuli. Alitoa changamoto kuwa "kama yupo mfanyabiashara yoyote alinichangia hata shilingi mbili tu asimame anyoshe mkono; nilikwepa kwa sababu nilitaka iwe kazi tu". Aliwahakikishia wafanya-

biashara wa Kitanzania kuwa wasiwe na wasiwasi wa kutaka kuingia kwenye shughuli yeyote ya maendeleo katika sekta yeyote ile. Akionesha kujibu mojawapo ya migogoro ya huko nyuma kati ya baadhi ya wafanyabiashara na Serikali iliyomtangulia Magufuli alisema kuwa "Hata ukitaka kuwekeza kwenye gesi au kwenye nini kwangu kuna nafasi". Aliongeza pia na kusema kuwa "hakuna nchi yeyote duniani ambayo haikuwasaidia watu wake wa chini; na ukiwasaidia na kuwajenga wazalendo wale wengine watakuja kuingia katika ubia. Huwezi kusema 'hawawezi hawawezi!' kwani wanaoweza wana damu ya namna gani" alisema na kusisitiza kuwa wafanyabiashara hao watangulize uzalendo.

Aliwataka wafanyabiashara ambao hawajalipa kodi wafanye hivyo. "Kwa wale ambao kwa bahati mbaya walikwepa hawakulipa ushuru na makontena wakayapitisha wasihangaie kuficha makontena; natoa grace period ya siku saba wakalipe kodi yao wakaishi kwa raha wala wasiwe na wasiwasi". Aliwaambia kuwa "kontena haliko kama sindano; ukilibeba huko mwishowe litakuponda bure. Nenda ukalipe katika kipindi hiki cha siku saba. Hata hivyo aliwaonya kuwa baada ya siku hizo saba kupita kuanzia Alhamisi hii basi sheria itafuata mkondo wake.

Aliwaambia – huku akishangiliwa – kuwa kama kuna mfanyabiashara yeyote anayetaka kufanya shughuli yoyote akajikuta anacheleweshwa na mtu yeyote na hasa kama mtu huyo yuko chini ya mamlaka yake ya uteuzi basi wajue kuwa mtu kama huyo hatokuwa na nafasi katika utumishi wa serikali yake. "Mtu huyo hatabaki kwenye Serikali yangu; kwa sababu huyo atakuwa anatuchelesha tunakotaka kwenda" alisema Rais Magufuli.

Aliwahidi kuwa wakati serikali yake inapanga bajeti ya 2016/2017 basi atahakikisha kuwa changamoto



TAHARIRI

mbalimbali ambazo wafanyabiashara hao ambao waliongozwa na Mwenyekiti wa Makampuni ya IPP Bw. Reginald Mengi basi atahakikisha zinaondolewa ili kuondoa urasimu na ukiritimba usio na sababu katika kufanya biashara nchini.

Aliwahakikishia wafanyabiashara kuwa pamoja na kuwepo kwa tofauti mbalimbali za kisiasa yeye "anawapenda" wote hata wale ambao hawakumpigia kura kwani kwa maneno yake mwenyewe "sisi sote ni Watanzania...tusahau yaliyopita tugange yajayo". Aliwaasa wafanyabiashara kutokutumia ukwasi wao kuminya haki za wanyonge hasa kwa vitendo kama kuvamia maeneo ya watu wengine au eneo la wazi au hata maeneo ya mapumziko. Aliwaambia serikali yake haitovumilia kuona wafanyabiashara wakitumia uwezo wao kununua maeneo ambayo siyo yao na aliwaambia kuwa kwa vile alishawahi kuwa Wizara ya Ardhi anajua madudu yaliyoko kwenye wizara hiyo.

Alisema wafanyabiashara wa Tanzania wamedhaurika vya kutosha sasa ifike mahali "tushike uchumi wa nchi yetu". Magufuli aliwahakikishia ushirikiano mkubwa kutoka serikali yake huku akiwapa changamoto ya kuunganisha nguvu zao kufanya mambo makubwa ya kuweza kuliinua taifa letu.

urithi wa vizazi vijavyo. Ni shamba ambalo tusipolilinda vyema na tukatunza mbegu kwa vizazi vijavyo tukajifanya tunataka kula mavuno yote leo - kwa kisingizio ati ni matamu sana' tunajilaani sisi wenyewe na uzao wetu.

Ndio maana tunamuunga mkono Magufuli; tunaunga mkono juhudi zote za kuwalazimisha walafi hawa wenye kula bila kutafuna kuwanyang'anya nafasi zao. Tutaunga mkono timua timua inayokuja na viongozi wazembe na wasio na uwezo; tunaunga mkono juhudi zote sahihi na za lazima za kutengeneza nchi yetu ilipoharibiwa.

Mpaka kila atakayeshika nafasi ya kuongoza ajue kuwa hili ni shamba lao, ni shamba letu, ni shamba ambalo hatuwezi hata usingizini kuliacha liwe shamba la wachache wenye kuamini wao ni zawadi kwa Tanzania. Juhudi zote hizo za kufanya shamba hili liwe bora, na litumikie Watanzania wa sasa na wa vizazi vijavyo kama urithi wao halali ni za kuungwa mkono. Hatuombeji juhudi zishindwe; na wala hatutarajia zishindwe.

Yeyote atakayejitangaza kuwa ni adui wa juhudi hizi basi huyu ni adui wa shamba letu.

KUTOKA OZ 2020: KUKATALIWA KWA LOWASSA

Baada ya uongozi wa CHADEMA kufanya kile ambacho wenyewe walikiita kuwa ni “kubadili gia angani” makundi ya Watanzania yaliambia na yenyewe kubadilisha gia ardhini.

Mtandao wa OZ uliundwa kwa kiasi kikubwa kama mwitikio wa uamuzi wa chama kikuu cha upinzani kuhodhisha na kudhoofisha harakati za mabadiliko kwa kuamua kumsimamisha mmojawapo wa watu ambao kwa tafakari ya kawaida kabisa alikuwa ni mwenye kugawa jamii.

Uamuzi wa kumsimamisha Edward Lowassa (pichani) kama mgombea

mgombea wa Urais kupitia kwamba yeyote aliyeonekana



CHADEMA na hivyo kuwakilisha matamano ya wapinzani na wapenda mabadiliko Tanzania ulifanywa kwa pupa, bila tafakari ya kutosha na uliongozwa na tamaa ya haraka ya kuingia Ikulu kiasi

kuhoji uamuzi huo alionekana na kuitwa msaliti wa harakati hizo—hilo likiwa ni jina zuri zaidi aliloitwa; mengine hayawezi kuandikwa humu.

OZ basi ilikuwa ni matokeo ya uamuzi huu. Mmojawapo wa wanaharakati wa mabadiliko na ambaye sauti yake imesikika mno katika miaka karibu ishirini hii anayetumia jina la M. M. Mwanakijiji hakuona haya wala aibu kuwa miongoni mwa watu waliokataa pendekezo hilo la wapinzani kwani lilikuwa lina kana na kudharau harakati zote za wapenda mabadiliko. Ndio kuzaliwa kwa OZ.

Wiki ijayo tutaanza kusimulia kwa kiasi kile ambacho kilifanyika kupitia matangazo ya youtube na sauti (audio) ambayo yalikuwa yanafanywa kila siku kwa muda wa wiki mbili mfululizo kuelekea uchaguzi mkuu wa 2015.

HABARI MAALUM: NDANI YA SIKU 100 TEUZI ZOTE MUHIMU?

Na. Mwandishi Wetu

Mojawapo ya mambo ambayo yanachelewesha kutangazwa kwa Baraza Jipya la Mawaziri ni pamoja na mipango ya kufanya mabadiliko makubwa katika safu mbalimbali za uongozi nchini ambayo yataendana na muundo na ujio wa baraza hilo jipya.

Kwa mujibu wa vyanzo vyetu vya ndani vyenye kututaarifu yanayoen-delea katika upangaji wa Baraza hilo, mojawapo ya vitu ambavyo

Rais Magufuli anaviangalia kwa umakini pamoja na wasaidizi wake ni safu nyingine za juu za viongozi wa kitaifa wa taasisi na vyombo mbalimbali vya serikali.

“Yeye Magufuli anataka kuhakikisha timu atakayofanya nayo kazi iwe ni mpya na ambayo inaanza pamoja kazi” kimetueleza chanzo kimoja cha kuaminiwa.

“Unajua kwa muda mrefu watendaji wengi wamekuwa ni wale wale na wamekuwa wakiendelea kutoka

utawala mmoja kwenda utawala mwingine lakini safari hii Magufuli anataka kufanya tofauti” kimeeleza chanzo hicho kwa masharti ya kutotajwa jina lake kwani hakikuwa kimepewa ruhusa ya kuli-zungumzia jambo hilo kwa waandishi.

“Ndani ya siku mia moja hivi za uongozi wake au zaidi ndani ya miezi mitatu Magufuli anataka kuwa amepanga safu yake vizuri ili kwamba mipango ya bajeti mpya

na maono mapya ya kitaifa yanapo-andaliwa basi yawe yanaandaliwa na watu ambao wanaelewana na wanailewa dhana ya serikali hii” kimemaliza chanzo hicho.

Kwa mujibu wa taarifa hizo, kama uchuguzi wa taarifa mbalimbali za watu utakamika mapema basi Baraza linaweza kutangazwa wakati wowote lakini vyovyote vile kwa mwendo uliopo linaweza kutangazwa Januari ili kuendana na kikao kijacho cha Bunge la Muungano.

JUKWAA LA HOJA: INAWEZEKANA KUTTIKIA “HAPA KAZI TU” KWA KUVUNJA SHERIA?

Na. F. M. Philip

UTANGULIZI

Falsafa ya utawala bora ndio nguzo ya serikali zote kwa sasa duniani, utawala bora katika nchi yoyote hupimwa kwa serikali yake kufuata na kuheshimu misingi ya haki za binadamu, utawala wa sheria, mgawanyo wa madaraka katika mihimili ya dola, uwazi katika uendeshaji wa shughuli za serikali na uwajibikaji wa viongozi wa serikali husika. Utawala bora

ndio msingi wa demokrasia iliyoko-maa popote duniani, kwani kwa sasa nchi zote duniani, mizania ya demokrasia yake hupimwa kwa kuzingatia uwepo wa utawala bora katika ngazi zote za utawala wa nchi, kuanzia serikali kuu hadi serikali za mitaa.

UTAWALA WA SHERIA (THE RULE OF LAW)

Neno “utawala wa Sheria” (the rule of law) halina maana moja iliyoku-balika kuwa ndiyo sahihi zaidi ya nyingine zote, maana ya neno hili

inaweza kutofautiana katika ya taifa moja na jingine na maana hii inategemea hasa tamaduni za kisheria (legal traditions) za taifa au mahala husika. Hata hivyo neno utawala wa sheria kwa ujumla wake linaweza kueleweka zaidi pale linapoelezewa kumaanisha utawala wa kisiasa unaofuata misingi ya sheria (legal political regime) ambapo sheria hutumika kuidhibiti serikali kwa kuhakikisha kwamba kunakuwepo na uhuru na haki kwa wanachi katika nchi na nidhamu ya utawala kuhusiana na

serikali inavyofanya kazi.

Katika kitabu chake cha (THE MORALITY OF LAW), mwanafalsafa Lon Fuller alitambua uwepo wa vipengele vinane muhimu vya kisheria vinavyotambulisha jamii inayofuata misingi ya utawala wa sheria:-

- Sheria zote kwa asili yake ziwe na mtazamo wa yajayo (laws should be prospective in nature) yaani sheria ianze kutumika tu pale ambapo imetungwa na kupitishwa, mfano mahakama

isimuhukumu mtu kwa kwa kutenda tendo amabalo halikuwa kosa kabla sheria husika haijapitishwa.

- Sheria lazima ziwepo na ziheshimiwe na wote ikiwemo serikali.
- Sheria lazima zifahamike kwa watu (laws must be published)
- Sheria lazime ziandikwe katika mfumo unaoleweka kwa watu ili kuondoa unyan-yasaji kwa watu wakati wa utekelezaji wa sheria hizo.
- Sheria isiwe inalazimisha lisilowezezana (law must not command the impossible)
- Sheria lazima iepuke mkan-ganyiko (law must avoid con-tradictions)
- Sheria lazima isimame imara muda wote ili kuruhusu kufahimika kwa kanuni zake, hata hivyo sheria lazima iruhusu mabadiliko kwa baadhi ya nyakati kulingana na mabadiliko ya kijamii na kisiasa katika nchi.
- Maamuzi ya watawala lazima yaendane na kanuni zilizopo (official action must be consistent with the declared rules).

Katika Tanzania yetu, hatuwezi kukataa kwamba nchi hii inatawali-wa kwa kufuata dhana hii ya uta-wala wa sheria, vigezo vyote alivyoweka Fuller katika falsfa yake vinazingatiwa, na Katiba ya Tanza-nia ya 1977 Ibara ya 26(1) (2) inazungumzia wajibu wa kufuata na kutii Katiba na sheria za Jamu-huri ya Muungano wa Tanzania kwa kila mtu na kuhakikisha katiba hii ambayo ndio msingi wa maisha ya jamii ya kitanzania inalindwa.

DHANA YA HAPA KAZI TU NA

KUTETEREKA KWA UTAWALA WA SHERIA

Jumapili ya tarehe 25/10/2015, iliku-wa ni siku muhimu sana kwa taifa la Tanzania na wananchi wake kwa ujumla, kwani siku hiyo ilikuwa siku ya uchaguzi mkuu wa wa viongozi wan chi katika ngazi za Rais, Wabunge na Udiwani. Kimsingi katika uchaguzi huu kilichokuwa kinashindanishwa ni sera za vya husika, na Chama cha Mapinduzi (CCM) kilifanikiwa kushinda kwa kishindo katika ngazi zote kuanzia Rais, Wabunge na Madiwani, kupitia mgombea wake Dr. John Pombe Magufuli (Tingatinga) aliyekuwa ame-beba kauli mbiu yake ya Hapa Kazi Tu.

Mara moja baada ya kuapishwa Rais Magufuli alithibitisha kwamba ameomba kazi ya urais kwa watanza-nia ili awafanyie kazi kama alivyowaahidi kwamba hata waan-gusha, aliyoyafanya katika kipindi hichi kifupi kwa taifa hili siyo ya kuelezeke na yameonyesha dira ya namna a anavyotaka viongozi wa chini yake wanavyopaswa kuwa yaani mawaziri, wakuu wa Mikoa na Wilaya katika mamlaka zao, na viongozi hawa baadhi wakiwemo wakuu wa mikoa na wakuu wa wilaya wameanza kuendana na kasi hii ya Mh Rais kwa kufanya kazi na kutoa amri, maelekezo mbali mbali yote ni kutokana na kauli mbiu hii ya serikali ya awamu ya tano ya Hapa Kazi Tu.

Katika kipindi kifupi sana cha utawala wake Mh Rais Magufuli tu-meshuhudia mabadiliko makubwa kwa watendaji na waajiriwa katika serekeli na sekta ya umma kwa ujumla kwani ile dhana ya kufanya kazi kwa mazoea katika utoaji hudu-ma kwa wananchi imeanza kubadili-ka kutoka na utekelezaji wa kauli mbiu hii ya Hapa Kazi Tu, tu-meshuhudia watumishi kadhaa wa ngazi za juu kwenye utumishi wa umma wasimamishwa kazi na wen-



gine kukabidhiwa nyadhifa mara moja, wengine wakifukuzwa, na wengine kuwekwa chini ya ulinzi kwa kuzembea kwa namna moja ama nyingine katika kutekeleza majukumu yao. Haya ni mambo chanya na yakuigwa kwa watawala na viongi wengine bila shaka, uchanya wake upo katika matokeo yake ya mabadiliko ambayo watan-zania wote tumekuwa tukiyatamani kila mmoja kwa nafasi yake.

Hata hivyo, katika kipindi hichi kifupi tangu kuanza kwa utekelezaji wa dhana hii ya Hapa Kazi Tu, tu-meshuhudia kwa kiwango kikubwa cha ukiukwaji wa misingi ya utawala wa sheria hapa nchini kutoka katika mamlaka za Mikoa hasa kwa baadhi ya wakuu wa Wilaya nchini kuitumia sheria ya Tawala za Mikoa Na. 19/1997 (The Regional Admin-istration Act No. 19/1997) kwa kutoa amri zilizo kinyume na matakwa ya sheria husika, huku amri hizo ziki-kiuka misingi ya utawala wa sheria na haki za binadamu na zingine kwenda kinyume na utawala bora pale amri hizo zilipoingilia mhimili mwingine yaani Mahakama, hivyo kukiuka misingi wa kikatiba wa mgawanyo wa madaraka katika dola ya Tanzania kama Ibara ya 4 (1) ya Katiba ya mwaka 1977 toleo la mwaka 2005.

Mifano mikubwa iliyochukua uzito katika habari za Tanzania siku ya jumatano ya tarehe 25/11/2015, wa kwanza ni kuhusiana na amri iliyo-

tolewa na mkuu wa Wilaya za Kinondoni Mkoani Dar Es Salaam Mh Paul Ma-konda (pichani juu) pale alipoamuru kuwekwa mahabusu kwa watendaji wa Ardhi wa wilaya hiyo ya kinondoni kwa kuchelewa kufika katika eneo la kazi walilokubaliana, kwa mamlaka aliyonayo kama mkuu wa Wilaya chini ya Kifungu cha 15(1) na (2) cha Sheria ya Tawala za Mikoa Na. 19/1997. Kilichofanya watu wahoji hapa ni je Mh Makonda alikuwa akielewa matakwa ya kifungu hichi na je matendo ya watumishi hawa yalikiidhi matakwa ya kutumika kwa kifungu husika na Mh. Makonda, na majibu yaliyotoka kwa wachambuzi mbali mbali wa sheria nchini yalithibitisha kwamba Mh Mkuu wa Wilaya ya kinondoni ndugu Paul Makonda alikitumia vibaya kipengele hicho cha sheria husika, hivyo kukiuka haki za maafisa hao kwa kuzuia uhuru wao pasipo sababu za msingi za kufanya hivyo kwani tendo walilofanya (kuchelewa kufika eneo la kazi) sio kosa la jinai na lina utaratibu wake wa kushughulikiwa kwa mujibu wa sheria ya Utumishi wa Umma (The Public Service Act) Na. 8/2002) pamoja na kanuni zake na sheria husika zinazo-husiana na masuala ya ajira na kazi.

Mfano wa pili ni kuhusu amri iliyotolewa na mkuu wa Wilaya ya Babati Mkoani Manyara inayohusu kukamatwa na kuwekwa mahabusu kwa Afisa mtendaji wa kata, mwenyekiti wa kitongoji na hakimumu wa Mahakama ya Mwanzo Basheti, lakini Mkuu huyo wa Wilaya ya Babati alienda mbali zaidi na kubatilisha amri iliyokuwa imetolewa na Mahakama

ya Mwanzo ya Wilaya hiyo kwa kurejesha mali(ardhi) iliyokuwa ifilisiwe kwa amri ya Mahakama hiyo. Amri hiyo nayo ilikuwa ni kwa mujibu wa kifungu cha 15(1) na (2) cha sheria ya Tawala za Mikoa Na. 19/1997.

Amri hii kimsingi ilikiuka kabisa misingi ya utawala bora kwani iliingilia mhimili mwingine wa dola (Mahakama ya Tanzania) hivyo ilikiuka lbara ya 107(B) inayotambua uwepo wa uhuru wa Mahakama (Independence of Judiciary) katika kutekeleza shughuli zake za utoaji wa haki, lakini pia amri ya kukamatwa kwa na kushitakiwa kwa hakimu huyo inaingilia kinga ya kutoshitakiwa ambayo Hakimu anayo wakati

akitekeleza majukumu yake Kisheria kama kifungu cha 66 (1) (a) na (b) cha Sheria ya Mahakama za Mahakimu Na. 11 marejeo ya mwaka 2002 na kimsingi kifungu hicho cha 66 (2) cha Sheria hiyo hiyo ya Mahakama za Mahakimu Na.11 marejeo ya mwaka 2002 kinawagusa maaafisa wengine waliokamatwa kwa amri ya Mkuu huyo wa Wilaya ya Babati, yaani Afisa mtendaji wa Kata na Mwenyekiti wa Kitongoji kwani katika kipindi wanatekeleza amri hiyo ya Mahakama sheria hiyo katika kifungu tajwa hapo juu inawatambua kuwa ni maafisa wa Mahakama, hivyo nao kama hakimu sheria imewapa kinga ya kukamatwa ama kushitakiwa kwa utekelezaji

wa majukumu ya Kimahakama.

Hii ni baadhi tu ya mifano ya amri na maamuzi ya watawala katika ngazi ya wilaya yaliyotawala vyombo vya habari katika siku kadhaa katika mwezi wa November 2015 amabapo amri hizo zilikiuka sheria mbali mbali za hichi kama zilivyoainishwa hapo awali. Wakuu hawa wa wilaya wanajibu kuonyesha jinsi wanavyoendana na kasi ya Mh Magufuli na kauli mbiu yake ya Hapa Kazi Tu. Amri hizo zilizotolewa na wakuu hao wa Wilaya zimeleta taharuki kubwa kwa wanaharakati wa haki za binadamu nchini na hoja kubwa inayojengwa hapa hapa ni jinsi dhana hii ya Hapa kazi Tu ina-

vyotekelezwa na watawala hawa katika ngazi za wilaya kuonyesha kutishia uwepo wa utawala wa sheria nchini Tanzania. Ni matumaini yangu na ya wananchi wa Tanzania kwa ujumla kwamba kasoro hizi ndogo zilizojitokeza katika utekelezaji wa dhana hii ya Hapa Kazi Tu zitafanyiwa kazi mapema ili kuepusha taharuki zisizo za lazima kwa mamlaka za serikali kwani hali hii ikiachiwa kuendelea na watawala hawa kundeleva kukiuka sheria za nchi katika kufanya maamuzi yao hasa yale yanayogusa haki za watu aidha mmoja mmoja au kikundi cha watu, tunaweza kushuhudia serkali ya awamu ya tano kuongoza kwa kushitakiwa mahakamani na wahanga wa amri na maamuzi ya watawala hawa katika mmalaka za Mikoa na Wilaya nchini.

SWALI AU JIBU: TUMEJIANDAA KWELI NA MABADILIKO?

Na Karegero Moses

Ni muda mrefu watanzania tumekuwa na kiu ya kutaka mabadiliko, harakati za mabadiliko si neno geni sana kwa wafuatiliaji wa maswala ya siasa hasa katika nchi yetu. Vuguvugu la mabadiliko lilianza mnamo mwishoni wa miaka ya 80 yakichagizwa na wanasiasa mahiri kama marehemu Mtikila ambao walijikita hasa katika muundo wa serikali inayopatikana katika kati-ba mpya.

Ni katika muktadha huo uchaguzi wa mwaka huu uliomalizika hivi karibuni wagombea wa vyama viwili vikuu vya upinzani ambavyo ni CCM chini ya Dk. Magufuli na CHADEMA chini ya Edward Lowassa walikuja na agenda ya kufanya mageuzi na mabadiliko makubwa sana katika uongozi wa nchi jambo ambalo lilionekana kulegalega katika awamu iliyopita kitendo kilichowakatisha tamaa wananchi wengi wa maisha ya kawaida.

Naomba nikiri wazi kabisa kuwa CHADEMA ile ya kabla ya kuingia kwenye uchaguzi mkuu ilionekana kubeba matumaini ya wanyonge walio wengi katika nchi yetu, ilijijenga kama taasisi na ilionekana kuchukizwa na

ufisadi uliokithiri sana katika nchi yetu. Katika kuona hilo CCM kama chama cha siasa kilijitathmini ili kuenenda na dhana ya mabadiliko na hivyo kikamsimamisha Magufuli maarufu kama "The Bulldozer" kiongozi ambaye anatenda anachoki- amini na kukiongea "Walks the Talk".

Kwa mantiki hiyo haikuonekana ajabu kwa waandishi maarufu na mahiri kama M.M Mwanakijiji kujitokeza na kupinga kile ambacho kilihubiriwa na aina ya watu wale wale waliotuletea matatizo makubwa sana ndani ya nchi kupitia CCM na hatimaye wakaamua kwenda upande mwingine tu ilimradi wafanikishe kitu walichokikusudia kwa muda mrefu wakitumia dhana ya mabadiliko "phantom changes" ili kuwateka wananchi wa chini kabisa.

Bila shaka na pasipo na shaka wengi tuliamini kuwa Dk Magufuli atachaguliwa kuwa rais wa JMT na ndo ilivyotokea huku watanzania wakisubiria mabadiliko makubwa katika utendaji wa shughuli za serikali. Watanzania wengine waliamini kuwa mabadiliko hayawezi kupatikana endapo tu CCM itaendelea kutawala, napenda niweke

wazi kabisa wengine (mimi) si waumini sana wa vyama hasa katika nchi zetu za kiafrica zilizojaa viongozi wenye tamaa na kiu ya madaraka, kuwa endapo chama fulani tu kikiingia au kutolewa madarakani ndo mabadiliko yataweza kupatikana, ninawakosoa wale tu ambao waliweza kuwaaminisha wananchi kuwa tatizo la nchi yetu ni CCM, yawezekana wengine walitaka CCM itolewe tu ili kudestabilize system iliyopo, cha kujiuliza ukishaiondoa CCM kwa kuweka watu walewale ambao hawakuwa na dhamira ya kufanya mabadiliko ya kweli ndo utalisaidia taifa? La hasha nchi kama China na Vietnam zimefanya mabadiliko makubwa kwa kufanya mabadiliko ya uongozi katika vyama vyao vya communist parties yaliyoletwa hasa na dhamira za viongozi wao katika kujenga nchi zao.

Naamini mabadiliko makubwa kabisa "radical changes" yatatokana na kurekebisha kwa baadhi ya sheria na hasa marekebisha katika katiba yetu ya sasa inayotoa dira ya kuendesha nchi yetu, mabadiliko hayo yatatuzesha kuwa na taasisi imara lakini mabadiliko hayo yatafikiwa kama

tutakuwa na kiongozi anayeweza kuishi katika anayoyaongea. Wiki tatu za Rais Magufuli ikulu zimetoa taswira ya jinsi nchi yetu itakavyoendeshwa na ule msembo wa business as usual nafikiri utakuwa umefikia kikomo. Hotuba ya Rais bungeni imetoa matumaini kwa watanzania waliokuwa wamepoteza matumaini ya nchi yao kuwa matatizo yao yawezekana yamepata mwarobaini na taratibu uzalendo utaanza kuwarejea watanzania na kumuunga mkono katika kufanikisha lengo kuu la kuupunguza umaskini na kuingia katika uchumi wa kati.

Kitendo cha Mh. Magufuli kutembelea sehemu mbali mbali kwa kushtukiza na kuwawajibisha baadhi ya viongozi ni katika kuboresha mazingira ya sasa "status quo" na hii inatoa taswira ya kuwa rais yupo concerned na matatizo yanaowakabili wananchi wa sasa, kwa maana nyingine inatupa picha kuwa hii ni nyakati nyingine na hivyo watanzania kwa pamoja tunatakiwa kufanya kazi kwa kujituma katika kufanikisha slogan ya HAPA KAZI TU, kwamba kila mwananchi katika eneo lake anatakiwa kufanya kazi yoyote halali kwa jitihada na maarifa.

KATUNI YA WIKI



SWALI NA JIBU: TUMEJIANDAA NA MABADILIKO?

Kwa muktadha huo ndiyo maana nimeuliza swali kuwa endapo watanzania tumejiandaa kwa mabadiliko tuliyokuwa tunayahitaji muda mrefu ,maana upokeaji na utekelezaji wa mabadiliko yoyote unategemea na uelekeo na utayari wa mtumiaji na mivuto mingine ,kwa maana nyingine; *adoption behavior is driven by behavioral intentions which are a function of an individual's attitude and the influence of external factors.*

Dk Magufuli kwa upande wake ameanza kufanya kazi yake ,katika ile hotuba ya kwanza kabisa ya kufungua Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliomba uungwaji mkono kutoka kwa wananchi katika vita dhidi ya rushwa na ufasidi maradhi ambayo yamelisumbua taifa kwa muda mrefu,alisema"Najua kutumbua jipu kuna maumivu lakini bahati mbaya halina dawa nyingine,hivyo ninawaomba waheshimiwa wabunge na watanzania wote kwanza mniombe na mniunge mkono ninapotumbua majipu haya"maneno mazito kutoka kwa



mkuu wa nchi, facial expression yake ilionyesha dhamira halisi ya serikali ya sasa katika kufanya mageuzi makubwa nchini.

Ni wajibu wetu watanzania wote hata wale waliokuwa wanampinga wakati wa kampeni tumpe ushirikiano Magufuli katika kuandika ukurasa mpya katika nchi yetu maana mapambano aliyoyaanza sasa yanawahusu hasa vigogo wakubwa wenye mtandao na mizizi mikubwa katika kuhujumu ustawi wa taifa letu ambao yawezekana walikuwa hawaguswi. Ni wajibu wetu pia kama watanza-

nia kutekeleza majukumu yetu katika sehemu zetu tunazofanyia shughuli zetu za kila siku, ni wajibu pia wa serikali kuwaelimisha wananchi hasa wasioweza kufikika kirahisi kuhusu dhana nzima ya mabadiliko na slogan ya HAPA KAZI TU .

Pichani juu wananchi wakishangialia ushindi wa Magufuli. Je ni kwa kiasi gani wananchi hawa wako tayari na wanajua maana ya mabadiliko ambayo yameanza kutokea? Je ni kwa kiasi gani wao wenyewe wamejiandaa kuwa tayari kuyaunga mkono siyo kwa kauli zao nzuri bali kwa kuitikia kwa vitendo maelekezo mbalimbali ya serikali hata kama yatakuwa ni ya usumbufu kwao? Je, itakuwaje kama wananchi wengi wanafikiria mabadiliko ni ya watu wengine?

KLHN NEWS INTL

Mchapishaji wa kijarida
hiki:

Wasiliana nasi:

klhnews@klhnews.com